An Phríomh-Oifig Staidrimh
Central Statistics Office

SWAHILI

# Sensa ya Idadi ya Watu Ireland

## Jumapili tarehe 10 April 2011

Fomu iliyotafsiriwa

**Sensa ya kuhesabia watu mwaka 2011**
Hii ni tafsiri ya maswali kwa Kiswahili ya fomu ya Sensa. Tafadhali tumia fomu hii kama ya kukusaidia kufirikiria na kujua maswali. Fomu yenyewe ya sensa ya kujaza majibu ni lazima sasa uijaze kwa kiingereza au Kiiarishi. Hii fomu itumie tu kwa kufirikiria na kujua majibu utakayoandika kwenye fomu yenyewe utakayoijaza kwa kiingereza au Kiiarishi.

**Kuhusu Sensa**
Sensa ya mwaka 2011 ya kuhesabia watu Ireland itafanyika Jumapili tarehe 10 Aprili (mwezi wa nne). Sensa itahesabia watu na kaya katika nchi hii usiku huo. Hii ni sensa ya ishirini na nne kufanyika toka ya kwanza iliyofanyia mwaka 1841. Matokeo ya sensa yatatoa picha kamili ya hali ya jamii na maisha na watu na itasaidia upangaji wa mipango ya mbele.

**Unatakiwa kufanya nini?**
Tafadhali weka fomu ya sensa mahali penye usalama na uijaze usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili. Usiku wa Sensa. Soma maelezo nyuma ya fomu kukusaidia kujaza fomu hii. Kumbuka kupiga sahihi tamko lilolo ukarasa wa 23 na uwe umeshajaza fomu yako tayari kwa kukusanywa na mhesabiaji wako.

**Wajibu wa kisheria kushiriki Sensa**
Hili ni tangazo chini ya kifungu cha 26 ya sheria ya takwimu ya mwaka 1993. Sensa hii inafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu ya mwaka 1993 na Takwimu( Sensa ya Idadi ya Watu) Amri ya 2010. Chini ya kifungu cha 26 na 27 cha Sheria ya Takwimu ya mwaka 1993 unatakiwa na sheria kujaza na kurudisha fomu. Mtu yeyoye anayeshindwa au kukataa kutoa taarifa au ambaye kwa makusudi anatoa taarifa za uongo anaweza kutozwa faini ya euro 25,000.

**Siri ya taarifa utakazotoa itahakikishwa na kulindwa**
Usiri wa taarifa ulizotoa kwa ajili ya sensa unalindwa na sheria ya Takwimu ya mwaka 1993. Ofisi kuu ya Takwimu itatumia taarifa ulizotoa kwa ajili ya takwimu tu. Hii ni pamoja na kutengeneza majedwali ya takwimu, taarifa za uchambuzi zaidi na kuchagua baadhi ya taarifa kuwa mifano.

**Muhesabiaji wako**
Muhesabiaji wako atakusaidia kama utakuwa na maswali au tatizo lolote kuhusu kuelewa au kujibu swali lolote kuhusu sensa. Tafadhali shirikiana kikamilifu na muhesabiaji wako ili kuifanisha Sensa ya mwaka 2011.

Asante kwa ushirikiano wako.

Gerard O'Hanlon
Mkurugenzi Mkuu

**Nani anaweza kujaza fomu ya sensa?**
Mkuu wa kaya au mtu mzima yeyote kutoka katika kaya husika atakayekuwepo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili. Fomu moja atajazwa kwa ajili ya kaya moja. Kila kaya moja itajaza fomu yake.

Maana ya **Kaya** moja ni:
- Mtu mmoja atayeishi peke yake au
- Kikundi cha watu wanaohusiana au wasiohusiana wanaoishi katika nyumba moja na kushirikiana mambo ya nyumbani kama kula walao mlo mmoja pamoja kwa siku, au wanaotumia sebule au chumba cha maongezi pamoja.

**Je utahitaji fomu zaidi?**
Kama kuna kaya zaidi ya moja katika nyumba moja mwombe mhesabiaji akupe fomu zaidi kadri ya kaya zinazoishi hapo.
Kama kutakuwa na watu zaidi ya 6 katika kaya mwombe mhesabiaji akupe fomu za bluu kwa ajili ya kila mtu mmoja anayezidi.

**Jinsi ya kujaza fomu yako ya sensa**
1. Tumia peni nyeusi au ya bluu.
2. Weka alama kwenye maboksi kama hivi
3. Kama ukifanya kosa fanya hivi kisha weka alama kwenye boksi sahihi.

Pale unapotakiwa kuandika jibu andika kwa HERUFI KUBWA na acha nafasi kati ya neno moja na jingine. Endeleza kuandika neno kwenye mstari unaofuatia kama halijamalizika kwenye mstari wa kwanza, kwa mfano:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H | O | T | E | L | | R | E | C | E |
| P | T | I | O | N | I | S | T | | |

**Andaa fomu yako kwa kukusanywa na kuchukuliwa**
Muhesabiaji wako atakuja Jumatatu tarehe 11 Aprili na Jumatatu tarehe 9 Mei kukusanya fomu mlizojaza.

Kama fomu yako haijakuchukuliwa na muhesabiaji mpaka tarehe 9 Mei, baada ya hapo itume ikiwa imejazwa kikamilifu kwa: Central Statistics Office, PO Box 2011, Freepost 4726, Swords, Co. Dublin.

# Maswali kuhusu unapokaa

**ANZA HAPA**

**H1 Kaya yako inaishi katika aina gani ya makazi?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu.*

**Nyumba nzima yaani:**

1 iliyo mahali pake peke yake
2 Iliyounganika na nyumba nyingine
3 Iliyounganika na nyumba nyingine zinazoshirikina kiwanja na uwanja mmoja

**Nyumba (au vyumba) iliyo katika nyumba moja ya ghorofa**

4 nyumba iliyo katika nyumba ya ghorofa
5 nyumba iliyo katika nyumba la ghorofa iliyobadilishwa kuwa ya kuishi au nyumba ambayo ni sehemu ya nyumba ya biashara

**Chumba:**

6 Chumba( ambapo ndani ya nyumba unatumia pamoja na watu wengine choo,au jiko au sebule)

**Nyumba zinazotembea au zilizojengwa kwa kutumia kwa muda mfupi :**

7 Nyumba zinazotembea kwenye gari(caravan) au nyumba zilizojengwa kama hema kwa ajili ya kutumia muda mfupi.

**H2 Nyumba au jengo unamoishi ilijengwa lini?**

*Weka alama katika mwaka nyumba au jengo hilo lilipojengwa kwa mara ya kwanza, na siyo mwaka liliobadilishwa au kuongezewa au kukarabatiwa..*

1 Kabla ya 1919
2 1919 – 1945
3 1946 – 1960
4 1961 – 1970
5 1971 – 1980
6 1981 – 1990
7 1991 – 2000
8 2001 – 2005
9 2006

**H3 Kaya yako inamiliki au inapanga na kulipia nyumba mnamoishi?**

*Weka alama katika boksi moja tu.*

1 Ninamiliki kwa kulipa mogeji(mortgage) au mkopo
2 Ni nyumba yangu silipi chochote
3 Ninapanga na kulipa kwa mwezi
4 Ninaishi hapa kwa msaada au fadhili silipi chochote

**Kama unapanga na kulipa kodi ya nyumba mpangishaji( landlord) wako ni nani?**

1 mtu tu binafsi
2 Serikali ya mtaa
3 Nyumba ya shirika au ushirika wa watu binafsi, dini, au watu wengine

**H4 Kama nyumba yako ni ya kupanga, kaya yako inalipa shilingi ngapi kama kodi ya nyumba?**

Weka kiasi unacholipa katika Euro.

€ ☐☐☐☐☐ • 0 0

*Weka alama katika boksi moja tu.*

1 kwa wiki
2 kwa mwezi
3 kwa mwaka

**H5 Vyumba vingapi wapangaji mnatumia katika nyumba hiyo ?**

- *Usihesabie bafu, choo, vyumba vya kuhifadhia vitu (stoo,) ofisi, duka, na vyumba vingine vinavyotumia kuwekea vitu.*
- *Hesabia vyumba vingine vyote kama jiko, sebule (chumba kikubwa cha maongezi katika nyumba, vyumba vya kulala, au sehemu ilijengwa kwa ajili ya kukaa pamoja au kusomea ndani au nje ya nyumba.*
- *Kama vyumba viwili vimebadilishwa na kugezwa kuwa chumba kimoja kikubwa kimoja hesabia kama chumba kimoja.*

Idadi au namba ya vyumba ☐☐

**H6 Mashine au mfumo wa kupasha nyumba joto unatumia nini?**

*Weka alama kwenye boksi moja*

1 Hakuna mfumo wa kupasha nyumba joto
2 Mafuta
3 Gesi ya asili( natural gas)
4 Umeme( Electricity)
5 Makaa ya mawe (pamoja na anthracite)
6 Masalia ya mimea (peat au turf)
7 Maji ya Gesi ya Petroli(Liquid Petroleum Gas, LPG)
8 Kuni za miti (pamoja na mbao ndogo ndogo)
9 Nyinginezo

**H7 Nyumba unapokaa inapata maji ya bomba kutoka wapi?**

*Weka alama katika boksi moja tu*

1 Kutoka kwenye bomba kuu la mji
2 Kutoka kwenye mradi wa maji ambayo chanzo chake kinamilikiwa na serikali ya mtaa au jimbo(county)
3 Kutoka kwenye mradi wa maji ambao chanzo cha maji kinamilikiwa na watu au kampuni binafsi kama (kama, Kisima kilichochimbwa, au ziwa, mto, n.k)
4 Kutoka kwenye miradi mingine ya maji binafsi kama, kisima, maji ya mvua, tangi la maji nk.)
5 Hakuna maji ya bomba

**H8 Nyumba unapokaa maji yaliyotumika (maji taka) yanatolewa vipi?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu.*

1 Mfumo au mtaro mkuu wa jumla wa kutoa maji machafu.
2 Tangi (tank) linalokusanya maji machafu lilipo nyumbani hapo
3 mfumo wa kuondoa maji machafu ulioyo katika nyumba ambao siyo wa kutumia tangi la maji machafu
4 Mfumo au utaratibu mwingine
5 Hakuna mfumo wa kutoa maji machafu

**H9 Kuna magari mangapi yanamilikiwa au yanatumiwa na watu katika kaya yenu**

*Hii ni pamoja na gari la kampuni ambalo unalitumia kwa matumizi yako binafsi*

*Weka alama katika boksi moja tu*

1 Moja
2 Mawili
3 Matatu
4 Manne au zaidi
5 Hakuna hata moja

**H10 Je katika nyumba yenu mna kompyuta?**

1 Ndiyo
2 Hapana

**H11 Katika nyumba yenu mmeweka na mnatumia internet?**

*Weka Alama 'Ndiyo' Kama mmeweka na mnatumia internet hapo nyumbani?.*

1 Ndiyo, tuna mfumo wa Broadband
2 Ndiyo, tuna mfumo mwingine
3 Hapana hatutumii internet

**H12** ▶ **Nenda Ukurasa unaofuatia**

## WATU WOTE LAZIMA WAHESEBIWE PALE WATAKAPOKUWA USIKU WA SENSA

**Hapo chini kuna makundi au orodha mbili. Kundi au Orodha ya kwanza 1 ni kwa ajili ya watu waliopo katika nyumba yenu usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi Aprili, 2010, USIKU WA SENSA. Kundi au Orodha ya pili 2 ni kwa ajili ya watu wanaoishi hapo nyumbani kwenu lakini ambao hawapo hapo nyumbani kwa muda na usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi wa Aprili, 2010.Angalia maelekezo kuhusu Swahili namba 7 nyuma ya fomu hii kwa maelekezo kuhusu maana ya mahali mtu anapoishi kwa kawaida.**

### WATU WALIOPO

**√ WANAOHESABIWA KATIKA KUNDI LA KWANZA**

- Watu wote walio hai ambao wapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi Aprili.
- Watu waliopo nyumbani kwenu kwa muda (kama, wageni au watu waliowatembelea).
- Watu waliofika Asubuhi ambao hawajahesabiwa mahali pengine.

**✗ USIWAWEKE HAWA KATIKA KUNDI LA KWANZA 1**

- Mtu yeyote anayeishi hapo nyumbani kwenu ambaye hayupo usiku wa sensa Jumapili tarehe 10 mwezi Aprili. Watu hawa utawaweka katika orodha au kundi na mbili2 la watu ambao hawapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili,
- Wanafunzi ambao hawapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi Aprili. Wanafunzi hawa waweke katika kundi au orodha namba mbili 2 ya watu ambao hawapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi wa Aprili
- Watoto watakaozaliwa usiku wa sensa saa sita usiku Jumapili tarehe, 10 mwezi Aprili

**KUNDI LA KWANZA 1 Watu WALIOPO nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili**

| Mtu No. | Jina la kwanza na Jina la familia au Ukoo |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| 5 | |
| 6 | |
| 7 | |
| 8 | |
| 9 | |
| 10 | |
| 11 | |
| 12 | |

Jibu maswali kuhusu kila mtu ambaye yupo nyumbani, Jumapili, terehe 10 mwezi Aprili kutoka ukurasa wa nne 4 kuanzia wa kwanza kama ulivyoorodhesha hapa.

Jibu maswali kuhusu mtu wa 7, 8, 9 na kuendelea. Andika maelezo kuhusu kila mmoja kwenye fomu za bluu. Kwa kila mmoja tumia Fomu yake. Fomu hizo utapata kutoka kwa muhesabiaji wako

### WATU WASIOKUWEPO

**√ WAWEKE KWENYE ORODHA AU KUNDI LA PILI LIST 2**

- Watu wote wanaoishi katika nyumba ambao hawapo nyumbani Jumapili tarehe 10 Aprili.
- Wanafunzi waliopo shuleni au chuoni.
- 

**✗ USIWAWEKE KWENYE ORODHDA AU KUNDI LA PILI LIST 2**

- Mtu yeyote uliyemuweka kwenye orodha au kundi la kwanza 1 hapa juu

**ORODHA au Kundi la pili 2 Watu mnoaoishi nao ambao hawapo nyumbani**

| Mtu No. | Jina la Kwanza na Jina la familia au ukoo |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| Kama kuna zaidi ya watu wanne 4 ambao hawapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili, tafadhali muulize muhesabiaji wako akuelekeze cha kufanya. | |

Jibu maswali kutoka ukurasa wa 22 kwa ajili ya kila mtu unayekaa naye nyumbani hapo ambaye hayupo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 mwezi Aprili

**1 Jina lako nani? (Mtu 1)**

*Jina lako na Jina la familia au ukoo.*

**2 Jinsia**

1 Mwanaume 2 Mwanamke

**3 Tarehe yako ya kuzaliwa ni lini**

Siku Mwezi Mwaka

**Swali namba nne 4 halimuhusu mtu wa kwanza( mtu 1)**

**4 Una husiana vipi na mtu 1?**

Uhusiano wa mtu 2 na Mtu 1

- Mume au Mke 1
- Mwenzi kama mume au mke ambaye hamjafunga ndoa au mnaishi kwa makubaliano (partner) hapa ni pamoja na wenzi wa jinsia moja) 2
- Mtoto wa kiume au Kike 3
- Mtoto wa kufikia au kambo 4
- Kaka au dada 5
- Mama au baba 6
- Babu au bibi 7
- Mama au baba wa kufikia au kambo 8
- Shemeji au wifi 9
- Mjukuu 10
- Uhusiano mwingine 11
- Hakuna uhusiano( hii ni pamoja na watoto, wa kulea -forster children) 12

**5 Taarifa kuhusu kuoa au kuolewa?**

*Jibu kama una umri wa miaka 15 au zaidi. Weka alama katika boksi moja tu.*

1 Sijao au kuolewa nipo mwenyewe
2 Nimeoa au nimeolewa mara moja
3 Nimeoa au nimeolewa mara ya pili( kufuatia kifo cha mume au mke wangu)
4 Nimeoa au nimeolewa mara ya pili( kufuatia talaka au kufutwa kwa ndoa
5 Nimetengana na mume au mke wangu(pamoja na kuachwa)
6 Nimepewa au nimetoa talaka
7 Ni mjane

**6 Ulizaliwa wapi?**

*Taja sehemu mama yako alipokuwa anaishi wakati unazaliwa*

Kama ni IRELAND (pamoja na Ireland ya Kasikazini) Andika jina la jimbo( COUNTY).

Kama hukuzailiwa Ireland andika jina la nchi. NCHI.

**7 Wapi unaishi kwa kawaida?**

1 HAPA katika nyumba hii
2 Mahali pengine IRELAND (pamoja na Northern Ireland)
*Andika anwani (Address) kamili ya nyumba unapokaa*

3 Nchi nyingine, Andika jina la NCHI

**8 Wapi uliishi mwaka mmoja uliopita?**

*Jibu kama umri wako ni mwaka mmoja na zaidi.*

1 HAPA napoishi sasa
2 Mahali pengine (hapa IRELAND Pamoja na Northern Ireland) Andika jina la JIMBO (COUNTY)

3 Nchi nyingine Andika jina la NCHI

**9 Umewahi kuishi nje ya Jamuhuri ya Ireland kwa mwaka mmoja au zaidi mfululizo?**

*Jibu kama umri wako ni mwaka mmoja na zaidi*

1 Ndiyo
2 Hapana

Kama **'NDIYO'**, Andika mwaka ulianza kukaa hapa katika Jamuhuri ya Ireland

NA

NCHI uliokaa mara ya mwisho.

**10 Wewe ni mtu wa taifa gani?**

*Kama una utaifa zaidi ya mmoja, tafadhali taja utaifa wako wote*

1 Mu-airishi
2 TAIFA nyingine andika hapo chini

3 Sina utaifa wa nchi yeyote

**11 Wewe in mtu wa asili au utamaduni gani?**

Chagua moja tu moja kati ya hayo hapo chini kutoka A mpaka D kisha weka alama kwenye boksi sahihi

**A Mzungu**

1 Muairishi
2 Muairishi msafiri (traveller)
3 Mzungu wa asili nyingine yeyote

**B Mweusi au Mwa- Irishi mweusi**

4 Mwafrika
5 Mweusi wa asili nyingine

**C Muasia au Muasia Mu-aIrishi**

6 Mchina
7 MwaAsia wa asili nyingine

**D Asili nyingine, pamoja na kuwa mchanganyiko**

8 Asili nyingine iandike

**12 Dini yako ni ipi?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu.*

1 Mromani Katoliki
2 Kanisa la Ireland
3 Mwislamu
4 Mpresbyteriani
5 Morthodoxi
6 DINI nyingine andika

7 Sina dini

**13 Umezaa watoto wangapi?**

*Swali ni kwa wanawake tu.*

Andika idadi ya watoto waliozaliwa hai.

1 sijazaa

**14 Unaweza kuongea Ki-airishi**

*Jibu kama una miaka mitatu au zaidi.*

1 Ndiyo
2 Hapana

**Kama 'Ndiyo', unaongea kiarishi mara ngapi?**

*Weka al;ama kwenye boksi moja tu*

1 Kila siku, mahali pa masomo
2 Kila siku, nje ya mahali pa masomo
3 Kila wiki
4 Mara chache tu
5 Hata mara moja

**15 Unaongea lugha nyingine zaidi ya Kiingereza au Kiarishi nyumbani?**

1 Ndiyo

2 Hapana ► **Nenda Swali 16**

**Lugha hii unayongea ni ipi?**

(mfano. KIPOLISHI, KIJERUMANI, KIAIRISHI LUGHA YA ALAMA)

**Kiingereza unaongea vizuri kiasi gani?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu.*

1 vizuri sana

2 Vizuri

3 siyo vizuri

4 Siongei kabisa

**16 Je una unasumbuliwa na matatizo haya ya kimwili?**

| | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|
| (a) Upofu au kuwa na shida kubwa ya kuona | | |
| (b) Ukiziwi au kusikia kwa shida sana | | |
| (c) Ugumu wa kufanya shughuli, kama kutembea, kupanda ngazi, kunyanyua na kuchukua vitu | | |
| Ulemavu wa akili | | |
| (f) Matatizo ya Kisaikolojia au hisia | | |
| (g) Matatizo ya maumivu, kupumua au ugongwa wowote usiopona kwa muda mrefu | | |

**17 Kama jibu lako ni 'ndiyo ' kwa swali lolote hapo juu kwenye swali namba 16, je una matatizo kufanya yafuatayo?**

| | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|
| (a) Kuvaa nguo, kuoga, au kutembea ndani ya nyumba | | |
| (b) Kutembea nje ya nyumba yako peke yako kwenda dukani au kwenda kwa daktari | | |
| (c) Kufanya kazi au biashara | | |
| (d) Kushiriki katika shughuli yeyote kwa mfano michezo kwa burudani au kutumia usafiri | | |

**18 Afya yako ipoje kiujumla?**

*Weka alama kwenye box moja.*

1 Nzuri sana

2 Nzuri

3 ipo sawa kiasi

4 Mbaya

5 Mbaya sana

**19 Unasafirije kwenda kazini, shuleni au chuoni?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu kwenye namna unayotumia kufika kazini , shuleni au chuoni*

1 siendi kazini, shuleni au chuoni

2 Kwa miguu

3 Baiskeli

4 Basi, au basi dogo

5 Treni, DARTI au LUASI

6 Pikipiki au Skuta(scooter)

7 Naendesha gari

8 Naendeshwa kwa gari

9 Vani

10 Namna nyingine, Lori, nk

11 Nafanyia kazi nyumbani zaidi

**20 Ni saa ngapi kwa kawaida unaondoka nyumbani kwenda kazini, chuoni au shuleni?**

1 Siendi kazini , shuleni au chuoni

2 Kabla ya saa kumi na mbili na nusu Asubuhi

3 kati ya saa kumi na mbili nusu na saa moja Asubuhi

4 kati ya saa moja na saa moja na nusu Asubuhi

5 kati ya saa moja na nusu na saa mbili Asubuhi

6 kati ya saa mbili na saa mbili na nusu Asubuhi

7 kati ya saa mbili na nusu na saa tatu Asubuhi

8 kati ya saa tatu asubuhi na saa tatu na nusu Asubuhi

9 Baada ya saa tatu na nusu Asubuhi

**21 Safari yako kwenda kazini, shuleni au chuoni inachukua masaa mangapi? Andika kwa dakika**

**22 Je unatoa msaada bila malipo kwa rafiki au ndugu katika familia yako mwenye ulemavu au matatizo ya muda mrefu ya kiafya?**

*Pamoja na matatizo ya uzee. Msaada binafsi ni pamoja kusaidia kumlisha au kumvisha nguo.*

1 Ndiyo

2 Hapana

**Kama 'Ndiyo', kwa masaa mangapi kwa wiki?** Andika masaa

**23 Kama upo chini ya umri ya 15**

► **Nenda swali 34**

**24 Umeacha kusoma shule?**

1 Ndiyo

2 Hapana

**Kama 'Ndiyo ', Andika Umri ulioacha kwenda shule.**

**25 Ni hatua ipi hatua ya juu kabisa ya elimu/ mafunzo uliofikia maliza mpaka sasa?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu*

1 Sijapata elimu ya darasani kabisa

2 Shule ya mshingi
Ngazi ya NFQ 1 au 2
*FETAC hatua ya 1 au 2, Cert. n.k*

3 Elimu ya Sekondari hatua ya mwanzo
NFQ hatua ya 3
*Junior/Inter/Group Cert., FETAC Hatua ya 3, n.k Cert., FÁS uangulizi wa ufundi, NCVA Kozi ya msingi (foundation) Cert, n.k*

4 Elimu ya Sekondari, hatua ya juu
NFQ hatua ya 4 or 5
*Leaving Cert. (Hii ni Pamoja na masomo ya ufundi,n.k*

5 Ufundi NFQ hatua ya 4 or 5
*FETAC hatua ya 4/5 Cert, NCVA Level 1/2, FÁS Ujuzi maalu, Teagasc Cert. katika Kilimo, CERT katika ufundi, n.k*

6 Cheti cha juu cha mafunzo kazini (Apprenticeship)
NFQ hatua 6
*Cheti cha juu chaFETAC, NCVA hatua ya 3, FÁS Cheti cha taifa cha ufundi., Teagasc cheti cha kilimo Cheti cha upishi n.k*

7 Cheti cha juu
NFQ hatua ya l 6
*cheti cha taifa cha NCEA/HETAC, n.k*

8 Digrii au shahada ya kwanza Diploma ya taifa
NFQ Hatua ya 7

9 Digrii au shahada ya kwanza ya heshima( hons.) Ujuzi wa kazi au vyote
NFQ hatua ya 8

10 Diploma baada ya digrii ya kwanza
NFQ hatua 9
Diploma baaya ya digrii ya kwanza, Digrii ya pili, nk

11 Shahada ya udakatri (Ph.D) au zaidi
NFQ hatua ya 10

**26 Ipi ni fani ya elimu ya juu kabisa ulivuzu au kumaliza mpaka sasa?**

*Acha shule ya sekondari*

Andika fani hiyo hapa

(Mfano. UHASIBU, MAMBO YA UREMBO UJENZI, UKULIMA, UFUNDI BOMBA)

**27 Hali yako kikazi sasa hivi ipoje?**

*Weka alama katika boksi moja tu.*

1 Nafanya kazi kwa malipo au kupata faida

2 Natafuta kazi yangu ya kwanza kabisa

3 Sijaajiliwa au sina kazi

4 Mwanafunzi au mwanachuo

5 Natunza familia nyumbani

6 Nimestaafu

7 Siwezi kufanya kazi kwa sababu ya ulemavu, au maradhi ya kudumu.

8 Nyingine, Andika

**28 Kama unafanya kazi, au hujaajiriwa au umestaafu ▶ nenda swali 29**

**Kama mwanafunzi ▶ nenda swali 34**

**Mwingeneo nenda ▶ swali 35**

**29 Una (uli) fanya kazi kama mwajiliwa au ume (uli) jiajili mwenyewe katika kazi yako kuu?**

Kazi yako kuu ni ile unayofanya kwa masaa mengi kwa kawadia

*Weka alama katika boksi moja tu.*

1 Mwajiliwa

2 Nimejiajili mwenyewe na nimeajili wafanyakazi pia

3 Nimejiali mwenyewe na sijaali wafanyakazi

4 Namsadia ndugu yangu (Sipokei mshahara maalumu)

**30 Kazi yako nini katika kazi yako kuu?**

*Tafadhali andika maelezo ya kazi yako ukitoa jina kamili la kazi yako na cheo chako.*

| Tumia majina kama | Usitumia majina ya jumla kama |
|---|---|
| MENEJA WA DUKA LA REJAREJA | MENEJA |
| MWALIMU WA SEKONDARI | MWALIMU |
| INJINIA WA UMEME | INJINIA |

*Watumishi wa serikali kuu na serikali za mahali waseme daraja mfano AFISA UTUMISHI MKUU. Maapolisi wa Gardaí au wanajeshi waseme vyeo vyao. Walimu waseme ngazi ya elimu wanayofundisha, mfano MWALIMU WA MSINGI. Watumishi katika mashirika ya dini waseme kazi zao kama, MTAWA*, NESI ALIYEANDIKISHWA NK.

Andika KAZI yako kuu

**Kama wewe ni mkulima** , Andika UKUBWA wa shamba lako katika hekari

Hekari

**31 Kama umestafu nenda ▶ swali 35**

**32 Nini biashara au shughuli ya mwajili pale unapo au ulipokuwa unafanya kazi?**

*Kama ume au ulikuwa ume jiajili mwenyewe (self-employed) jibu kuhusu kazi au biashara yako.*

*Elezea kitu au hudumu kuu inayotolewa na mwajiri wako.*

Kwa mfano, KUTENGENEZA KOMPYUTA, KURABATI MAGARI,ELIMU YA SEKONDARI, MAUZO YA CHAKULA, KUTENGENEZA MADAWA, KUSAFISHA MAJENGO, UJENZI NA KUTOA MSAADA KWA WAJENZI, KUANDIKA PROGRAMU ZA KOMPYUTA.

**33**

**Kama huna kazi sasa ▶ Nenda swali 35**

**34 Taja JINA KAMILI NA ANWANI ya mahali unapofanya kazi, kwenda shule au chuoni**

**Jina kamili**

**Anwani**

1 nafanyia kazi nyumbani 2 Sina mahali rasmi napofanyia kazi, nafanyia kazi popote

**35 Jibu maswali kuhusu Mtu 2 kutoka ukarasa unaofuatia**

**Kama ni mtu mmoja tu hayupo nyumbani usiku wa tarehe 10 Aprili nenda ▶ ukarasa wa 22**

# Watu ambao unaishi katika kaya ambao hawapo nyumbani siku ya sensa

**Jibu maswali A1 mpaka A8 kwa ajili ya watu wote wanaoishi katika kaya yenu ambao hawapo nyumbani usiku wa Jumapili, tarehe 10 Aprili. Usisahau kuwaandika wanafunzi waliopo shuleni au chuoni, ambao watakuwa hawapo nyumbani usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili**

**Mtu ambaye hayupo nyumbani**

**A1 Jina lake nani?**

*Jina la kwanza na jina familia au ukoo.*

**A2 Jinsia**

1 Mwaume 2 Mwanamke

**A3 Alizaliwa tarehe gani?**

Siku Mwezi Mwaka

**A4 Mtu huyu ana uhusiano gani na mtu 1 mwenye maelezo ukurasa wa nne?**

*Weka alama kwenye boksi moja tu*

1 Mume au mke

2 Mwenzi unaiyeishi naye kama mume au mke ambaye hamfunga ndoa(partner) hapa ni pamoja na wenzi wa jinsia moja)

3 Mtoto wa kiume au wa kike

11 Namna nyingine ya uhusiano, andika uhusiano huu

12 Hakuna uhusiano (Pamoja na watoto waliochukuliwa kutunzwa)

**A5 Hali ya mtu huyu kuhusiana na kuoa au kuolewa?**

Jibu kama umri wako ni miaka 15 au zaidi

*Weka ⊖ alama kwenye boksi moja tu*

1 hajawahi kuoa wala kuolewa

2 ameoa au ameolewa(pamoja na wale walioa au kuolewa mara ya pili)

5 Ametengana (pamoja na wale walioachika)

6 Ametariki au amepewa talaka

7 Mjane

**A6 Huyu mtu hajakuwepo nyumbani muda gani?**

1 Pungufu ya miezi kumi na mbili

2 Zaidi ya miezi kumi na mbili

**A7 Huyu mtu alikuwepo katika Jamuhuri ya Ireland Jumapili tarehe 10 Aprili?**

1 Ndiyo

2 Hapana

**A8 Mtu huyu ni mwanafunzi ambaye yupo chuoni au shuleni??**

1 Ndiyo

2 Hapana

**Tamko au kiapo cha kufanywa na mtu aliyejaza fomu hii**

**Kabla ya kupiga sahihi tafadhali angalia:**

- Kwamba umejibu maswahili kuhusu mahali mnapokaa ukarasa wa 2.
- Kwamba katika Orodha au kundi la kwanza 1 kwenye ukurasa wa tatu 3 umejaza maelezo ya watu wote (pamoja na wageni) ambayo walikuwepo nyumbani kwenu usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili.
- Kwamba umejibu maswali yote yanayotakiwa kujibiwa kuhusu kila mtu aliyekuwepo nyumbani kwenu usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili ( kutoka ukurasa wa 4-21)
- Kwamba katika Orodha au kundi la kwanza 2 ukurasa wa tatu 3,umejaza maelezo kuhusu watu wanaokaa kwenye nyumba yenu ambao hawakuwepo nyumbani Jumapili tarehe, 10 Aprili.
- Kwamba umejibu maswali yote ukurasa 22-23 kuhusu watu katika kaya yako ambao hawapo kwa muda usiku wa Jumapili tarehe 10 April.
- Kwamba hakuna mtu amehesabiwa mara mbili kwenye fomu.

Nathibitisha kuwa fomu imejazwa kikamilifu na ni sahihi kwa kadri upeo na ninayojua na imani yangu

Sahihi yako

**Asante kwa kujaza fomu ya Sensa.**
**Asante kwa ushirikiano wako.**

**Kama kuna watu zaidi ya wanne 4 ambao hawapo nyumbani kwenu usiku wa Jumapili tarehe 10 Aprili muulize muhesabiaji wako kwa maelekezo.**

# MAELEKEZO YA KUKUSAIDIA KUJAZA FOMU

**Swali H3 – Je kaya yako ina miliki mahali mnapoishi au nyinyi ni wapangaji?** Kama mnapanga hapo na kulipa kodi ya nyumba (boksi 3), au mnaishi hapo bila kulipa kodi ya nyumba (boksi 4), Jibu pia sehemu ya pili ya swali 'Nani anawapangisha nyumba au nani ndiye mwenye nyumba?'. Chagua boksi lilosahihi(1, 2 au 3) kusema kwamba mpangishaji au mmiliki wa nyumba yenu ni ' Mtu binafsi, 'Serikali ya mtaa au mahali' au 'Shirika au ushirika binafsi, kama mashrika ya dini' hata kama unalipa sehemu tu au kodi nzima ya nyumba au hata kama kodi hiyo inalipwa kwa ajili yako na HSE au shirika jingine lolote.

**Swali H4 – Kama mahali unapokaa umepanga kaya yenu ina inalipa kodi ya kiasi gani?**
Kama HSE au shirika nyingine lolote linalipa sehemu ya kodi ya nyumba andika kiasi kile tu mnacholipa nyinyi. Andika kiasi hicho kwa makadirio kamili katika Euro kufuatana na jinsi mnavyolipa, kwa mfano, kama kaya yako inalipa kodi ya nyumba Euro 78.60 kwa wiki andika Euro 79 na weka alama kwenye boksi 1. Kama kodi yenu yote inalipwa kwa ajili na shirika fulani andika 0 na weka alama kwenye boksi 1.

**Swali 4 – Uhusiano**
Swali la uhusiano limewekwa kutambua familia katika kaya. Hii ni pamoja na pale ambapo kuna familia mbili au zaidi katika kaya. Kwa mfano kaya yenye binti au mtoto wa kike mkubwa anayeishi na wazazi wake wawili na yeye ana mtoto wake mmoja, kaya hii itahesabika kuwa na familia mbili.

Mfano uliotolewa hapo chini unaonyesha jinsi ya kujibu swali kuhusu mtoto katika hali hii pale ambapo wazazi ni Mtu 1 na mtu 2 katika fomu, binti au mtoto wa kike mkubwa ni mtu 3 na mtoto wake ni Mtu 4.

Weka alama ⊟ kwenye boksi moja kwa kila mtu

| Uhusiano kati ya MTU wa 4 kwa | | Na mtu 1 | 2 | 3 |
|---|---|---|---|---|
| Mume au mke | 1 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mwenzi unaiyeishi naye kama mume au mke ambaye hamjafunga ndoa au mnaishi kwa makubaliano(partne) hapa ni pamoja na wenzi wa jinsia moja) | 2 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mtoto wa kiume au wa kike | 3 | ☐ | ☐ | |
| Mtoto wa kufikia au wa kambo | 4 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Kaka au dada | 5 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mama au baba | 6 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Babu au bibi | 7 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mama/baba wa kufikia au wa kambo | 8 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Shemeji au wifi | 9 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mjukuu | 10 | ⊟ | ⊟ | ☐ |
| Uhusiano mwingine | 11 | ☐ | ☐ | ☐ |
| Hukuna uhususiano (pamoja na watoto wanachukuliwa kutunzwa) | 12 | ☐ | ☐ | ☐ |

**Swali 7 – Wapi unaishi?**
Swali hili linahusu mahali ambapo unaishi kwa kawaida mpaka wakati wa sensa hii. Kama umeishi hapo mfululizo kwa kipindi cha walau miezi 12 kabla ya usiku wa sensa au umefika hapo walau katika kipindi cha miezi12 kabla ya usiku wa sensa na una nia na unataka kuendelea kukaa hapo kwa kipindi cha walau mwaka mmoja zaidi weka alama katika boksi1 (HAPA). Kama mahali unapokaa kwa kawaida si hapa bali sehemu nyingine hapa Ireland (pamoja na Ireland ya Kaskazini, Northern Ireland) weka alama katika boksi 2 na andika anwani (address) kamili ya hapo unapokaa. Kama mahali unapokaa kwa kawaida ni nchi nyingine kabisa weka alama katika boksi 3 na andika jina la nchi hiyo unayokaa.

Maelekezo ya kiujumla ni kwamba mahali pa kawaida anapoishi mtu ni pale anapopumzika kila usiku. Maelekezo yafutayo yatumike,

- Wale ambao huwa hawapo nyumbani kwao wakati wa siku za wiki na ambayo huwa wanarudi kwenye nyumba ya familia yao wikiendi (weekends) wachukulie nyumba ya familia yao ndiyo mahali pao pa kawaida pa kuishi.
- Wanafunzi wa shule ya msingi ambao wanakaa shuleni na wale walio vyuoni wahesabie nyumba ya familia yao kama ndiyo mahali pao pa kawaida wanapoinshi.
- Kama mtu amekaa au anategemea kukaa kwenye taasisi fulani kwa muda wa miezi 12 mtu huyu achukulie taasisi hiyo ndiyo mahali pake pa kawaida pa kuishi.
- Kama mtu anaishi mahali zaidi ya pamoja mara nyingi katika mwaka, basi mahali anapotumia muda mwingi katika mwaka ndiyo achukulie kama mahali pake pa kawada pa kuishi.

**Swali 8 – Mwaka mmoja uliopita wapi uliishi kwa kawaida?**
Hili swali linawahusu watu wenye umri wa mwaka mmoja au zaidi. Maelekezo kuhusiana na swali 7 pia yanalihusu na yatumike kwa swali hili. Kama mahali pako pa kawaida pa kuishimwaka mmoja uliopita kabla ya Sensa bado ni hapo hapo ulipo sasa weka alama katika boksi 1 (SAWA kama sasa-SAME as now).

**Swali 9 – Umewahi kuishi nje ya Jamuhuri ya Ireland kwa muda wa mwaka mmoja au zaidi mfululizo ?**
Swali hili linawahusu watu wenye umri wa mwaka mmoja au zaidi. Kama mahali pako pa kuishi pa kawaida ni katika Jamuhuri ya Ireland.na kama:

- Ulizaliwa katika nchi hii na umekaa nje ya nchi hii kwa kipindi cha mwaka mmoja au zaidi mfululizo.
- Ulizaliwa nchi nyingine na kuishi nje ya Ireland kwa kipindi cha mwaka mmoja au zaidi weka alama katika boksi 1 (Ndiyo). Pia andika mwaka wa mwisho ulipokuwa mkazi katika nchi hii na nchi uliyoishi mara ya mwisho.

**Swali 15 – Unaongea lugha nyingine zaidi ya Kiingereza au Ki-a Irishi nyumbani kwako hapa?**
Kama unaongea lugha nyingine ambayo siyo Kiingereza au Ki-airishi nyumbani kwako hapa weka alama katika boksi 2, kisha endelea na swali 16. Hii ina maana wale wanaongea Kiingerereza na Ki-aIrishi nyumbani kwao hawahitaji kusema uwezo wao wa kuongea Kiingereza.

**Swali 16 – Je una moja ya hali au matatizo yafuatayo ya kudumu?**
Kwa ajili ya swali hili hali au tatizo la kudumu ni tatizo au hali ambayo mtu amekuwa nalo au anategmea kuwa nalo kwa muda wa miezi 6 au zaidi au ambalo linatokea mara kwa mara.

**Swali 22 – Je unatoa msaada bila malipo kwa rafiki au mtu wa familia yako mwenye maradhi, matatizo ya kiafya au ulemavu?**
Kama unatoa msaada bila malipo mara nyingi kama mtunzaji hata kama unapokea au hupokei posho au malipo mengine yeyote kama mtunzaji(carer) weka alama katika boksi 1( Ndiyo-Yes) na andika namba ya masaa unayotoa msaada kwa kwa wiki.

**Swali 25 – Nini kiwango au hatua ya juu la elimu/ mafunzo uliyofikia mpaka sasa?**
Madaraja au viwango mbalimbali ya elimu vilivyowekwa katika swali hili vinafuata Mfumo wa Taifa wa Sifa na Viwango vya Elimu( National Framework of Qualifications (NFQ). Maelezo zaidi yanapatikana hapa (www.nfq.ie)

Maelezo zaidi kuhusu FETAC, HETAC, na sifa nyingine za elimu kutoka hata nje ya hapa na sifa nyinginezo kiumjula zinapatikana hapa (www.census.ie)

**Swali 26 – Nini ni somo au utalaamu wa kiwango cha juu cha elimu ulifikia mpaka sasa?**
Hili swali linahusu elimu au masomo uliosoma baada ya elimu ya shule ya sekondari peke yake. Kama umemaliza kozi kadhaa na una sifa za elimu katika fani au masomo mengi taja moja ambayo umepata elimu ya juu kuliko zote.

**Swali 27 – Unailezeaje hali yako ya sasa kuhusu kazi?**
Weka alama kwenye boksi moja tu linaloelezea vizuri na vema zaidi hali yako kuhusu kazi sasa.Kama upo likizo au likizo baada ya kupata mtoto weka alama kwenye boksi 1 (Nafanya kazi-Working).

**Swali 34 – Anwani( Address) ya mahali unapofanya kazi, kwenda shule au chuoni**
Watu wanaondoka kwenye kaya kwenda kufanya kazi, kusoma shule au chuo waandike anwani ( address) kamili ya mahali wanapofanya kazi au kusoma.

Kwa watoto wahudhuria shule ya chekechea(mfano crèche, kindergarten) nje ya nyumbani kwao, andika jina kamili na anwani( address ya hapo wanapokwenda kusoma.